



KONGAMANO LA ISHIRINI NA TISA LA KISWAHILI BAYREUTH

Tarehe 6 Mei hadi 8 Mei 2016

13 Novemba 2015

Wapendwa washiriki,

Kwa furaha tunawatumieni ujumbe huu kuwafahamisheni kuhusu kongamano lijalo na kuwakaribisha tena hapa Bayreuth katika Kongamano la ishirini na tisa la Kiswahili ambalo tunalitayarisha kwa sasa.

Kongamano la Kiswahili

Kongamano la Kiswahili limeshaota mizizi hapa katika Chuo Kikuu cha Bayreuth. Mwaka baada ya mwaka, tunajumuika na wataalamu mbalimbali wanaojishughulisha na uchunguzi wa vipengele kadha wa kadha vinavyohusu Kiswahili na tamaduni zake. Msingi madhubuti ulilo nalo kongamano hili, umepatikana kutokana na upana wa mada zinazozungumziwa mwaka baada ya mwaka; kuanzia isimu, masomo ya fasihi mpaka anthropolojia na historia, kwa kutaja chache tu. Kongamano hili ni fursa ya wataalamu kutoka pembe mbalimbali za dunia hupata kubadilishana mawazo. Kwa wajao kila mwaka karibuni sana. Kwa wataalamu, wanafunzi na mashabiki wapya, msisite hata kidogo kupanga kuja kuwasilisha au kuhudhuria tu.

Mada kuu za Kongamano la 2016

Kongamano hili linalenga kumulika mada mbili kuu.

Ile ya kwanza ni **Jazanda na Mitazamo: Nguvu ya Taswira katika Dunia za Kiswahili**. Katika moja ya makala ya Micere Mugo, ambayo imenukuliwa mara nyingi na wengi, Mugo anaeleza jinsi taswira ya mhusika *kibibi kizee kichawi Gagula* kitaka riwaya ya Haggard, *Mashimo ya Mfalme Sulemani*, ilivyomletea kupatwa na hofu na woga mkuu akutanapo na wanawake wazee wa Afrika. Mfano huu unaonyesha wazi jinsi taswira za sanaa zinaathiri urazini wetu. Taswira za kila aina zikumbwa zinaathiri mazoea yetu katika maisha yetu ya kawaida na pia zinaathiri uhalisia wa jamii. Kutokana na mtazamo huo, badala ya kuangalia sanaa kama kioo cha jamii kama ilivyofanywa mara nyingi, tunataka kupendekeza mtazamo ambao unasisitiza kwamba taswira lugha, fasihi na sanaa zenyewe zinazaa maana ambazo zinaweza kuathiri jamii. Kwa hivyo, mnakaribishwa kuchambua lugha, fasihi na sanaa nyingine ili tujadili vipi hizi zinaleta maana kwa sitiari na ishara. Vipi dhana nzito, kama mapenzi, nyumbani, maumivu, kifo, zimetafsiriwa kwa sitiari na jazanda? Lugha ya

Kiswahili inatumia sitiari gani ya kukuzia na kuchambulia au kufasiria dhana tete za kihisia na kuzinyambua ili zieleweke kwa urahisi (k.m. wakati, nafasi, hisia)? Na vipi sitiari na taswira zinaathiri maisha ya kila siku? Kwa mtazamo wa kihistoria: vipi taswira, ishara na jazanda zitumiwaje upya na kufasiliwa tena na tena? Kwa namna gani taswira zinaza maana?

Mada ya pili inatokana na majadiliano mengine ya Kongamano la mwaka huu na panel yake itaandaliwa pamoja na Dr. Maud Devos (Royal Museum for Central Africa, Tervuren): **Utofauti wa kilugha katika maeneo ya Kiswahili**. Ikilinganishwa na lugha nyingine za Afrika, kwa upande mmoja, Kiswahili kimefanuliwa vizuri pamoja na lahaja na rejesto zake. Kwa upande mwingine, bado kuna majadiliano makubwa kuhusu maswala ya kimisingi kama vile uainishaji wa lahaja za Kiswahili, nafasi na mipaka yao ndani ya familia ya lugha za ki-Bantu na uhusiano na lugha ambazo ziko karibu. Vilevile majadiliano haya yanahu masuala ya kihistoria kama kuenea kwa Kiswahili na wazungumzaji wake, uanzishaji wa lahaja na rejesto na mandeleo yao. Zaidi ya hayo, maeneo mengine kama vile hali ya lugha katika ncha ya kaskazini na ya kusini ya lahaja za pwani za Kiswahili haikuzingatiwa sana, sawa na hali ya maeneo ya barani Kenya, Tanzania, Uganda na Kongo na nje ya Afrika. Kuhusu maswala haya, tutapenda kupokea michango mipyä kuhusu “Viswahli” na uhusiano wa Kiswahili na lugha zilizo jirani na michango ambayo inaangalia upya tafiti zilizopo za historia ya isimu. Pia michango ya isimu-jamii na ya fasihi ambayo inaonyesha athari za lugha jirani ama lahaja inakaribishwa sana.

Hata ingawa mada tulizozieleza hapa juu ndizo mada kuu za kongamano la 2016 na zitatupa vipengele vya kupangia mijadala yetu, pia tunakaribisha wasilisho na mapendekezo yenye mada nyingine, kwa sababu Kongamano la Kiswahili la Bayreuth linalenga nyanja tofauti na vile vile ni fursa iliyo wazi kwa michango yoyote ile inayohusu Kiswahili na Waswahili kwa jumla. Kwa mfano, tungependa kuwapatia walimu wa Kiswahili nafasi pia ili wapate kujadiliana masuala yao pia.

Usajilishaji

Tunawaomba mutoe makala katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kila uwasilishaji wa mada pamoja na majadiliano utapewa muda wa dakika thelathini tu (dakika kumi ya hizi zikiwa ni za majadiliano). Tafadhalini tumieni baruapepe ili kujiandikisha (kwa swahili@uni-bayreuth.de) na mtutumie kichwa cha awali cha makala yenu mapema iwezekanavyo. Mwisho wa kutuma ni **tarehe 20 mwezi wa Februari mwaka wa 2016** ili tuwe na fursa ya kuandika ratiba ya kongamano. Iwapo utawasilisha kwa Kiswahili, tafadhalii ututumie na muhtasari wa makala kwa Kiingereza. Tunawaomba wote kujiandikisha hata ikiwa mtashiriki bila ya kuwasilisha makala.

Pahala na Wakati

Pahala pa Kongamano hili ni **Iwalewa-House**, kituo cha masomo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Bayreuth, iliyo katika Wölfelstraße 2, 95445 Bayreuth.

Mwaka wa 2016 Kongamano la Kiswahili litaanza asubuhi ya siku ya **Ijumaa tarehe 6 mwezi wa Mei** na litamalizika **Jumapili tarehe 8 Mei**. Tunatayarisha habari zaidi, kama vile, ratiba na barua ya mwaliko, ambazo mtaweza kuzipata hivi karibuni katika anwani ifuatayo mtandaoni:
http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html

Mwanzoni mwa mwaka ujao tutawatumieni habari zaidi kwa njia ya baruapepe. Ikiwa mna maswali, msisite kutuandikia. Kwa mawasiliano zaidi, tumieni anwani yetu ya: swahili@uni-bayreuth.de

Tunawatakieni wakati mzuri tukiwa na matumaini ya kuonana nanyi katika Kongamano la 29 la Kiswahili hapa Bayreuth.

Salamu nyingi,

Prof. Dr. Clarissa Vierke & Nikitta Adjirakor, Fred Bosire, Roberto Gaudioso, Serena Talento

Literaturen in afrikanischen Sprachen

Universität Bayreuth,

95440 Bayreuth

Tel.: +49-921-553550

Fax.: +49-921-553641

swahili@uni-bayreuth.de

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/de/colloq/swahili_colloq/index.html